

# **Uthibitisho: Vikombe Siyo Maandiko**

**Na**

**E. H. Miller**

**1946-1952 (?)**

# **Uthibitisho: Vikombe Siyo Maandiko**

**Na**

**E. H. Miller**

**1946-1952 (?)**

“Wale wanaotumia vikombe vingi wanaweza kuabudu nasi na wasiende kinyume na Biblia au dhamira, hatuwezi kuabudu pamoja nao bila kwenda kinyume na wao, sasa tufanyeje kuhusu hilo.”

— E.H Miller —

(Marko 7:7-9; Gal. 1:8-9; Rum.16:17-18; Kumb.12:32; Hes. 22:18; Ufu. 22:14-19; 2Tim.3:13-17)

# Kikombe cha Bwana

Kuna watu wengi leo wanao laani vikombe na vikundi katika kanisa, lakini pia kuna wanao laani vikundi kuliko vikombe; kiukweli, vikundi vingi vinanyo laani wanajaribu kudhihirisha vikombe katika Meza ya Bwana. Lakini kwa nini ulaani kimoja na huku umeshikilia kingine? Hata hawezi kupata katika neno la Mungu lilo barikiwa.

Oh! Mtu mmoja akasema, Mimi siyo wa vikombe, kwa sababu chombo hakina sehemu katika Meza ya Bwana: “ Ni uzao wa mzabibu ndio unaoitwa kikombe, na nikikombe bila kujali jina au idadi ya vyombo iliyo ndani yake.” Sawa Biblia inasema, 1Wathes. 5:21, “*Jaribuni mambo yote,*” sasa nataka mtu athibitisha hilo kama wanaweza.

Ndiyo, wanasema, Kristo alisema “Kikombe hiki ni damu yangu” na tunajua kuwa chombo si damu yake, ila uzao wa mzabibu; kwa iyo hicho ndicho Kristo aliita kikombe. Sasa hiyo inashawishi, lakini kuna tatizo moja; Kristo hakusema “**Kikombe hiki ni damu yangu.**” Kauli hii haiwezi kupatikana katika kurasa za Biblia, ila kile ambacho Kristo alisema inapatikana katika Luka 22:20, “*Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu.*” Sasa Agano jipya sio damu ya Kristo; vile vile Damu ya Kristo siyo kikombe iliyo tajwa katika Luka 22:20 kwa sababu hiyo “*kikombe ni agano jipya katika Damu yake.*” Lakini hii inamaanisha nini? Hebu tusome mustari huu katika toleo zingine na tuone kama hatuwezi kuelewa vizuri. Toleo la mwendo mzuri: *Kikombe hiki ni makubaliano inayothibitishwa na damu yangu.*” Toleo la Morffat inasema: *hiki kikombe kina maanisha agano jipya, inayothibitishwa na damu yangu.*” Na kitabu cha Thayer Lexicon ya Kiyunani-Kiingereza cha Agano Jipya, kwa kuelezea mustari huu katika ukasa wa 15 inasema yafuatayo, “Maana ni” “*kikombe hiki kilicho na uzao wa mzabibu, ni ishara ya damu, inatolewa kwa kumwaga damu kama ishara ya Agano Jipya.*” Sasa marafiki, hebu muwe wa kweli ninyi wenyewe, mvinyo huo ulikuwa kwenye chupa au kikapu? Hapana, ilikuwa kwenye kikombe, kama wengi wanavyoweza kuona. Na Thayer alisema kuwa kikombe kilikuwa ishara ya Agano Jipya na mvinyo ulioko ndani ya kikombe ilikuwa ni ishara ya damu ya Yesu, na kuwa damu hiyo, ilifunikwa na Agano Jipya ambayo iliwakilishwa na kikombe iliyokuwemo, kama nilivyo thibitisha kupitia Matha. 22:20.

Lakini hebu na tusome msitari mwingine, Math.26:27, “*akakitwaa kikombe akashukuru, akawapa akisema, nyweni nyote katika hiki.*” “Huwezi kunywea chombo.” Sawa hebu na tuone.

# JE TUNAWEZA KUNYWA KIKOMBE?

Marazote, vikombe vywetu ndugu zangu inaonyeshwa katika 1Wako. 11:25-28 na inasema: “ hatuwezi kunywa chombo, vile vile neno ‘kikombe’ haimaanishi chombo, kwa vile hapa inaeleza, ‘ *kunywa kikombe hiki na nywea kikombe kile*’, tusingeweza kufanya hivyo kama kikombe inamaanisha chombo. Sawa hebu na tuangalie kuhusu swala hili. Fungua name katika Ezek.23:32, na tusome: “*Bwana MUNGU asema hivi, utakinywea kikombe cha umbu lako, chenye nafasi nyingi kikubwa; utadhahiwa na kudharauliwa; kimejaa sana.*” Sasa unaona kuwa hiki “kikombe” kilikuwa na nafasi nyingi na kikubwa, na kuwa kimejaa sana. Je yeyote anaweza kukataa kuwa hiki “kikombe” kinacho zungumziwa hapo juu ni **chombo?** Kumbuka kuwa **kimejaa sana** na yakuwa kina **nafasi nyingi na kikubwa.**” Hii inawezaje kuwa tu kimiminio? Tafsiri pana ( toleo lililo endelea la tafsiri ya wabapstist) inasema: *hivyo asema Bwana Yehova, utakinywea kikombe cha umbu lako, ambalo ni pana na kina nafasi nyingi,*” na mustari wa 34 inasema: *na utakinywea na kukimaliza chote.*” Kutokana na hicho hapo juu, hakuna mtu ambaye ni mkweli atakataa kuwa chombo hakizingatiwi, kwa maana kumbuka: “*ilikuwa imejaa sana ,*” kilikuwa “ na nafasi nyingi na kikubwa, walipaswa kunywa wamalize,” na ilikuwa na nafasi nyingi,” na Mungu akasema “*mnyweni*” na *mnywee.*” Wanaweza kumtii Mungu? Au Mungu aliwaambia kufanya isiwezekane? Hapana! Wangefanya kile Mungu alisema, vile vile na sisi pia. Lakini tunawezaje kunywa kikombe? “*Kwa kunywa kile ambacho kipo ndani ya kikombe*”-Thayer, na “*kwa kunywa kile ambacho kipo ndani ya kikombe*”-N.I Clark, kila mmoja anapaswa kufahamu. Walikinywea kwa kunywa kile ambacho kilikuwa ndani ya kikombe, na tuna kunywa kikombe cha Bwana, kama jinsi walivyo nywea kikombe cha umbu lao. Tukirudi nyuma katika Matha. 26:27, tusome mustari huu katika toleo zingine au tafsiri zingine, kama maranyingine wanaifanya rahisi kuelewa. Toleo la Diaglott, “*Mnyweni nyote toka kwalo*” toleo iliyo na mwendo mzuri, “*alichukua kikombe cha mvinyo- akisema lazima nyote mkinywee.*” Kwa hiyo unaona, ilikuwa ni kikombe cha **mvinyo** Kristo alinywea, na wote **walikinywea.** Lakini sasa ikiwa bado una mashaka na neno “*kikombe*” hapa inazungunzia chombo, hebu tuangalie Thayer (Yule Yule ambaye watu wa vikombe wanamuendea, kujifunza batiza inamaanisha nini) na katika ukrasa wa 510 ya kitabu chake cha Lexicon tunasoma, “*chombo amabacho mtu anatumia kwa kunywa, Math. 26:27,*” ukrasa wa 533-“*kikombe, chombo cha kunywa, Math. 26:27.*” Kwa hiyo unaona yakuwa huyu msomi wa Kiyunani ambaye wote wanamuendea kutafuta maana ya neno, anatuambia “kikombe”, katika Math. 26:27, ilikuwa ni kikombe chombo cha kutumia kwa kunywa,” “*ambacho mtu anatumia kwa*

kunywea” na katika toleo la Diaglott katika Marko 14:23 inasema, “*wote walikinywea.*” Kwamba mkuu wa wanafunzi, R.F Weymouth, katika Agano Jipya lugha ya kisasa, anaitoa, “ na wao, wote, walikinywea”; na pongezi ziko katika maneno ya pembeni (“kutoka kwa”). Ikionyesha kuwa wote walikinywea kikombe hicho hicho, kama ilivyo fanywa katika sherehe ya kifizikia “wakati ambapo “kikombe cha Upendo” kinapitishwa kwa wote.

Hebu na twende katika kamusi ya Biblia na William, D.D, ya mwaka 1859, “kikombe- Neno hili linachukuliwa katika Biblia kihalisi na kimfano pia. Katika mtazamo wa halisi, inaonyesha kikombe cha kawaida cha pembe au chuma chochote chenye thamani (Mwanz. 40:30; 1Wafal. 7:26), kama ambavyo inatumika katika kunywea wakati wa chakula; au kikombe cha sherehe, au chakula cha kidini, kama katika Pasaka, wakati baba wa mji alipotangaza baadhi ya Baraka juu ya kikombe, baada ya kuionja, aliipitisha kwa watu wote, wasaidizi wake na kwa familia kwa ujumla, ambao wote walikinywea (Luka 22:16; 1 Wakor. 10:16)” Sasa, kikombe hiki cha sherehe ilikuwa ni nini ambayo walikinywea wakati wa Pasaka? Ebu natusogee mbele kidogo katika kitabu hiki hiki na tuone Mwandishi wa Kiyunani anatupa maelezo kamili ya sherehe ya pasaka, ambapo tunapata wazo. Wale waliotakiwa kushiriki baada ya kufanya utakaso uliyoitajika na wakiwa wamekusanyika mezani, mkuu wa sherehe alichukua kikombe ambacho kina mvinyo, na akamshukuru Mungu kwaajili ya uzao wa mzabibu ambamo wote walinywea.” Kwaiyo tunaona wakati wa chakula cha pasaka wakati Kristo alianzisha meza ya Bwana wote walinywea kikombe kimoja cha uzao wa mzabibu, na kikombe hiki na kilichokuwemo viliitwa kikombe cha Baraka kama jinsi ninavyo kwenda kuonyesha hapa. Ebu na tukumbuke kauli katika “Maisha na wakati wa Yesu Masihi” na Alfred Edersheim, M.A Oxon, D.li, Ph. D., ukrasa wa 497 na 511”- Kristo anaonekana amepitisha kikombe kimoja kwa wanafunzi wake- hii iliitwa na mtakatifu Paulo, ( 1 Wakor.10:16) kikombe cha Baraka.” Kwaiyo rafiki yangu, unaona kikombe cha Baraka katika 1 Wakor.10:16 ilikuwa ni kikombe cha uzao wa mzabibu, ambamo wote walinywea kwalo. Hapa pia naweza nika nukuu kitabu cha Dummelow, 1 Wakor.10:16, kikombe cha Baraka kikombe ambacho Baraka ziliombwa kwalo.” [ kulingana na desturi za kiyahudi na historia kulikuwa na vikombe vine vya uzao wa mzabibu usiyo chachwa katika meza ya Pasaka; Wayahudi wote walinywea vikombe vitatu vya kwanza; hawakukinywea kikombe cha nne; ilifunikwa katika sahani iliyokuwa tupu ambayo ilitunzwa kwa ajili ya Masihi ( wengine husema ilitunzwa kwa ajili ya Eliya, ambaye waliamini angeweza kurudi kabla ya kuja kwake Masihi). Kikombe cha kwanza kilichotumika kiliitwa Kiddush, ambayo inamaanisha utakaso. Kikombe cha pili kilichotumika kiliitwa

*kikombe cha mapigo*. Kikombe cha tatu kiliitwa *kikombe cha ukombozi*. Kikombe cha nne kilitunzwa kwaajili ya Masihi kiliitwa *kikombe cha Baraka*. Paulo alifahamu desturi za Kiyahudi na sheria, akiwa amesoma chini ya miguu ya Gamalieli (Matnd. 22:3); hii ndiyo maana alikuwa akimaanisha kikombe tunayotumia katika meza ya Bwana (1 Wakor. 10:16) kama *kikombe cha Baraka*, kwasababu hicho ndicho Bwana alitumia wakati Alipoanzisha Meza yake kutoka katika Pasaka – Ellis Forman]

Unahitaji uthibitisho zaidi? Sawa, tugeukie historia ya Agano Jipya” na Harris Franklin Roll, rais wa Liff shule ya Biblia, ukrasa wa 155-“ tukifuata mapendekezo ya maneno ya Paulo yaliyoandikwa miaka michache baadaye ( 1 Wakor.11:23-25), kiongozi angelichukuwa kikombe cha uzao wa mzabibu na kuongeza: *vivyo hivyo kikombe pia baada ya chakula, akasema kikombe hiki ni Agano jipya katika damu yangu: fanyeni hivi kila mnywapo kwa ukumbusho wangu.*” Kwaiyo unaona Yule aliesubiri katika meza ya Bwana wakati wa Paulo alichukua kikombe cha uzao wa mzabibu, sio chupa ya pombe, au kikombe chochote cha pombe.

Hebu na tugeukie concordance (kitabu)ya Agano Jipya na la Kale, “kikombe- hili neno linatumika; (1) neno kwa neno, kikombe kilicho tengenezwa ambalo mtu anatumia kwa kunywa; na (2) lugha ya mfano, kwa ajili ya kitukinacho husu kikombe (1 Wakor. 11:27). “kwaiyo tena, tunapata **kikombe** na siyo chupa au vikombe Fulani vilivyotumika katika Meza ya Bwana. Lakini hebu subiri kwanza! Mtu mmoja akasema, hukutambua alisema kikombe cha 1 Wakor.11:27 ili maanisha **fahirisi kwaajili ya kikombe?** Ndiyo, nimegundua hilo, “ fahirisi ya kikombe” siyo fahirisi ya chupa au vikombe Fulani. Kwaiyo kama unataka kuita uzao wa mzabibu kikombe, ni lazima iwe **fahirisi ya kikombe**. Na hii itathibitishwa zaidi kwa kutembelea kitabu cha Universal Dictionary.” Kwa nini tuna kamusi? Kujifunza kile maneno inamaanisha, sivyo? Sawa, hebu na tuangalie kitabu hiki na tuone “kikombe” inamaanisha nini. Kikombe – 1. Chombo ndogo, ilitumika mara nyingi kunywa; kikombe cha kunywa mvinyo sanasana chombo cha mfinyanzi iliyotengenezwa wakawekea pa kushika na ilitumiwa na mpishi kama; kama kikombe cha chai; kahawa. 2. Fahirisi ya kikombe ni kile ambacho kimo ndani ya kikombe; kama kikombe cha kahawa. 3. Chombo ambacho mvinyo wa sakramenti huwekwa; pia mvinyo wenyewe.” Kwaiyo hapa tena tunapata kikombe kihalisi kikombe au fahirisi. Kahawa huitwa kikombe **pale inapokuwa ndani ya kikombe**, lakini kama ikiwa ndani ya chungu inayochemka, ungeweza kusema chungu inachemka sawa na kusema rejeta haina maji; ukizungumzia maji ndani ya rejeta. Kwaiyo, kikombe kwa muungano na Meza ya Bwana inamaanisha kikombe au kishikio kinacho shikilia mvinyo, na

mvinyo ndani ya kikombe hiki au kishikio huitwa kikombe kwasababu ni fahirisi **ya kikombe**. Lakini kishikio ni nini? Tuta ruhusu kamusi hii itufafanulie, Kishikio- kikombe cha kunywea au gudulia; hasa kikombe cha ushirika.” Kwaiyo unaona maranyingi tuna hitimisha **na chombo** kwa muungano na Kikombe cha Bwana, na chombo hicho ni **kikombe**, sio baadhi ya vikombe au chupa kwaajili ya mvinyo ingeweza kuitwa chupa kama ingekuwa ndani ya chupa. Unaitaji uthibitisho? Sawa, angalia neno chupa katika kamusi hii, “Chupa- 1. Kifaa ambacho kina tundu refu, ubao, ngozi, au kifaa kingine, ambayi inamdomo mwembamba; kwaajili ya kubebea kimiminio. 2. Kifahirisi ya chupa; kwaiyo mvinyo ndani ya chupa, huitwa chupa lakini ndani ya kikombe huitwa kikombe, na Biblia inatuambia katika Marko 14:23 *“alitwaa kikombe na baada ya kushukuru, akawapa na wote wakakinywea,”* tafadhali tambua alitwa kikombe (umoja). **Ilikuwa ni kikombe kabla haja kitwaa,** na akawapa kile alichochukua (umoja), **“ wote wakakinywea.”**

Sasa kumbuka tayari nimeshaonyesha jinsi walivyo kinywea, lakini pia nitakupa uthibitisho zaidi kwa kunukuu mistari ileile kutoka katika toleo zingine. Kwanza, toleo la Diaglott, *“na kuchukua kikombe, baada ya kushukuru, akawapa, na wote wakakinywea”* sasa kutoka katika toleo mwendo mzuri, **alichukua kikombe cha mvinyo** na akashukuru na akawapa na wote wakakinywea.” Marafiki, tafadhali kumbukeni kwamba Kristo alichukua **“kikombe (umoja), cha uzao wa mzabibu”** na akawapa (kikombe cha uzao wa mzabibu)” na wote **wakakinywea,**” kutoka katika kikombe cha uzao wa mzabibu akwapa. **Aliwapa kikombe kimoja na wote wakakinywea.**

Labda haitawezekana kupata kazi za wasomi wakubwa zaidi ya kitabu cha nukuu ya Mathayo na mtu maarufu wa Ugiriki, John A. Broadus. Na haya ndio maneno yake *“ alichukua kikombe”* (umoja)-kikombe ndilo neno zuri hata katika Mathayo na Marko, wakati Luka na Paulo wanakiita *“kikombe”*. Kulikuwa na kikombe mezani cha kunywea mvinyo kulingana na desturi ya chakuli cha wayahudi *“kikombe”* hakisemi kuwa kulikwa na vikombe vingine.”[ Tena, kulikuwa na vikombe vinne katika pasaka, lakini ni moja tu iliyotunzwa kwaajili ya Masihi. – Ellis Forsman]

Sasa unaona jinsi ilivyo rahisi na vyepesi kuthibitisha kikombe kimoja katika Meza ya Bwana kupitia Biblia, kamusi au historia, na kwavile haiwezi kuthibitishwa kwa vivyo vovyote vile kwamba chupa au vikombe ni salama, ebu tuendele na vitu ambavyo tumeshajifunza na imehakikishwa katika (2 Tim. 3:13-19).

Kwa faida ya wale ambao hawajaridhika, ebu tuendeleo kidogo kiundani katika somo hili. Katika kamusi iitwayo karne mpya, toleo la 1,

ukrasa wa 361- “kikombe....pia imetumika, kikombe na fahirisi yake, kiwango ambacho kilikuwa ndani ya kikombe.” Maandishi ya pembeni na Thomas Scott, D.D., katika Biblia takatifu iliyotolewa 1818 inayosema hivi katika 1 Wakor. 10:16, “kikombe cha uzao wa mzabibu” ambayo ilitumika kwenye Meza Ya Bwana kuwakilisha Baraka za kiroho; Math.26:27, uzao wa mzabibu ndani ya kikombe hicho iliwakilisha damu yake, iliyomwagika ili kutengeneza njia kwa ajili ya Agano Jipya. Hakuna maneno ya nyongeza inayoitajika ili kuonyesha vikombe vingapi vilitumika.

Sasa angalia katika kitabu kikubwa kiitwacho Encyclopedia Americana, toleo la 6 ukrasa wa 252: kikombe cha maombolezo ambamo mvinyo uliyo takasika ulikuwemo. Ya kwanza kabisa kati ya hizi ilikuwa na kishikio, kwa jinsi yalivyokuwa **mapana na mazito.**” Yasingekuwa mapana na mazito kama makanisa hapo awali yalitumia vikombe vingi. Hebu natusome moja ya hivi vikombe katika Encyclopedia ya kisasa chini ya neno “chalice” kikombe cha maombolezo mvinyo ulitunzwa mtu mmoja aitwaye Charlemagne alitoa chombo hiki cha dhahabu iliyokuwa na uzito wa kilo 53, kwa Mtakatifu Petro kule Rumi.” Labda hii ilikuwa ni kwa ajili ya kusanyiko lililo na maelfu ya waumini, ni kikombe ambacho ndugu wameliongelea zaidi.

Lakini tugeukie Agano Jipya la Kiyunani lililo na mandishi ya Kingereza na J. A. Spencer, A. M., iliyo hariwa na Harper &Brothers, mwaka 1868. Chini ya Marko 14:23 tunasoma, “katika pasaka wageni wote walinywea kikombe hicho icho.” Kikombe **kwa** Kiyunani ni “**poterion**” na tutaona kile ambacho kitabu cha Thayer cha kiyunani na kiingereza, inasema hapa. Ukrasa wa 533, **Poterion-kikombe, chombo cha kunywea-** Math.26:27; Marko 14:23; Luka 22:17; 20; 1Wakor. 11:25.” Thayer anasema “kikombe” katika mistari hii akimaanisha chombo cha kunywea. Ukrasa wa 510, “ chombo ambacho mtu anatomia kwa kunywea, Math. 26:27; Marko 14:23.” Pia anasema katika ukrasa wa 189, **kitu ambacho mtu anatomia kwa kunywea,** Math.26:27; Marko 14:23; 1Wakor. 11:28.” Tena katika ukrasa wa 15, “ 1 Wakor. 11:25; Luka 22:20 **hivi vyote vinamanisha, kikombe hiki kilicho na uzao wa mzabibu, ni ishara ya damu, inayotolewa kwa kumwagika damu yangu ni ishara ya Agano Jipya.**” Kwaiyo anatuambia kikombe iliyotajwa katika Math. 26:27; Marko 14:23; Luka 22:20; 1 Wakor. 11:25 na 1 Wakor 11:28 ni “**chombo iliyo na uzao wa mzabibu**”, uzao wa mzabibu ni ishara ya damu ya Kristo, na chombo walivyotumia kwa kunywea ni ishara ya Agano Jipya.

Kamusi ya Biblia ya Smith iliyoandikwa na William Smith, D. C., L.L. D., ambayo watu wengi wanaamini kwa kutafsiria maneno ya Biblia, katika kitabu kiitwacho complete unabridged edition iliyo na toleo tatu na zaidi ya kurasa 4,156, inayozungumza kuhusu pasaka, “Mvinyo



haujatajwa kwa muungano na Pasaka katika vitabu vya Agano la Kale. Lakini Mishna kimadhubuti inseam kuwa hakupaswi kuwe na zaidi ya vikombe vine iliyotolewa katika chakula cha sherehe, hata kwa Muisraeli maskini (Pes 10:1). Vikombe vilitolewa kwa mzunguko na utaratibu malum wakati wa chakula. Inaonekana viwili vimeonyeshwa katika Luka 22:17, 20. Kikombe cha Baraka ( 1 Wakor. 10:16) yamkini baadaye ilikuwa mojawapo ya hizi kiujumla cha tatu [ cha nne hawakukinywea, kilitunzwa kwa ajili ya Masihi- Ellis Forsman] katika mtiririko.” Unaweza kuona kuwa kikombe cha Baraka (1Wakor.10:16) ilikuwa ni kikombe chenye mvinyo. Lakini mtu anaweza kuuliza kama hawakutumia vikombe vine katika Pasaka. Ndiyo, lakini Kristo alitumia moja kati ya hizo katika meza ya Bwana, kikombe cha Baraka, cha tatu [cha nne] kikombe cha mvinyo ambamo wote walikinywea wakati wa Pasaka [ kilitumiwa tu na Bwana-EF]. Wote walinywea katika kila vikombe vine wakati wa Pasaka lakini pia wote walikinywea kikombe cha Baraka wakati Meza ya Bwana. Katika toleo la 2, ukrasa wa 139-140, Smith anaongea kuhusu kuchunguza pasaka-“ mkuu wa kaya, au mshereheshi, anaanza na mtindo wa Baraka kwa ajili ya siku na mvinyo, iliyotangazwa juu dhidi ya kikombe. (sio chupa EHM) ambamo yeye na wengine wanakinywea.” Kumbuka, wote walinywea kikombe hicho. Sasa endelea, “meza iliandaliwa nje na kondoo wa kuchomwa, mkate usio chachwa, mboga chungu na sahani zilizo fahamika kama charoeth.

Washereheshi kwanza, baadaye wengine, walichovya mboga chungu katika bakuli hili ( charoeth) na kula. Sahani ziliondolewa, na kikombe cha mvinyo kikaletwa tena- kikombe kilipitishwa kwa kila mtu akakinywea. Kumbuka hii ilikuwa ni “**kikombe cha mvinyo**” na **wakakinywea kikombe**. Baadae walikula nyama ya kondoo aliyeokwa, kwa mkate [ ni mkate usio chachwa ndiyo ulitumika katika pasaka-Ellis Forsman] nk., jinsi walivyopenda, na baada ya hapo Baraka nyingine, kikombe cha tatu, iliyofahamika kama kikombe cha Baraka, [ kikombe cha Baraka ilikuwa ni kikombe cha nne na hakikupitishwa kwa kila mtu-Ellis Forsman] walipewa mkononi wakawa wanapokezana. Hii ilisaidiwa na kikombe cha nne.” Wote walikunywa katika kila kikombe wakati wa Pasaka, na kikombe cha tatu ambamo wote walikinywea kilitwa “kikombe cha Baraka.” Kikombe hicho kitumika katika meza ya Bwana. [kumbuka, kulikuwa na kikundi cha wayahudi waliochukulia kikombe cha tatu kuwa ni cha Baraka, lakini hawakufuata desturi ya kutunza au kuweka kikombe cha Baraka katika sahani tupu ya Masihi- Ellis Forsman]. Kamusi ya Biblia iliyoandikwa na William w. Rand, 1859, inasem ilikuwa ni “kikombe” cha mvinyo usio chachwa”. Na hapa tunaweza kuongeza, kwa faida ya wale wanao shindania mvinyo ulio chachwa, kwamba Biblia haitufundishi kutumia pombe katika meza ya Bwana. Vilevile mbele yangu ninakaratasi

inayopingana iliandikwa na W. F. Jones katika maandishi ya pembeni wakati wa mwezi wa kumi, 1941, pale alipobisha kuwa tunatakiwa kutumia mvinyo mkali (pombe). Anasema, “ walikuwa na kinywaji iliyoagizwa, mvinyo mkali (pombe), uzao wa mzabibu, kinywaji ambayo haija chachwa iliyo tumiwa mara zote katika sherehe za Agano la Kale, sadaka, Pasaka, na Bwana akiwa katika meza yake usiku ule aliyo salitiwa... Wayahudi- sawasawa- walikatazwa wasiwe na chachu katika nyumba zao wakati wa sherehe ambayo inafanana na pasaka yetu. Angalia anavyojichanganya mwenyewe. Kwanza alisema kuwa walikuwa na uzao wa mzabibu, kinywaji ambacho hakija chachwa iliyo tumiwa na Bwana katika Meza yake usiku ule aliyo salitiwa...kwaiyo hatuwezi kuwa na mvinyo ambao hauja chachwa. (???) Alafu hatuwezi kuwa na kile Kristo alitumia?? Hapaswi kujuwa kuwa isiyo chachwa inamaanisha, haijawekwa amira, na haijawekwa amira inamaanisha haijachachwa. Anapaswa kuangalia katika kamusi ya Webster ili kunyambua maneno haya: Isiyotiwa amira- “haijaumuliwa...haija chachwa.” Iliyowekwa amira- “imechachwa”. Kitabu cha Thayer cha Kiingereza na Kiyunani cha Agano Jipya inatafsiri hivi: kuchachua, ni kuchanganya chachu na unga ilikuifanya iumke.” Kitabu mtu ayeitwa Young, ukrasa wa 596, inatupa tafsiri ya hili neno “chachwa” kwa Kiyunani: kituchochote iliyo chachwa au iliyo wekwa amira.” Kwasababu wana wa Israeli hawakuweza kutumi au kuwa na chachu wakati wa pasaka, ila walipaswa kutumia vitu visivyo chachwa au kuwekwa amira, walitumia mvinyo usio na amira kama jinsi kamusi ya Biblia ilivyosema. Soma Math.26:29 katika tafsiri ya kitabu kiitwacho mwendo mzuri (Good speed), “ *Nitakunywa uzao mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu.*” Uzao mpya ni nini? Isaya 65:8, “*Bwana asema hivi kama vile divai mpya ipatikanayo katika kichala.*” Divai hii itakuwa haijachachwa kwa amira. Maelezo ya pembeni ya Agano Jipya iliyotafsiriwa na Ferrar Fenten, M.R.A.S., M.C.A.A., chini ya Math. 26:27-29, “ itakiwa ifahamike kuwa hakuna kinywaji iliyo na amira ambayo ingeweza kutumiwa na Waebrania wakati wa wiki ya pasaka.” Mtu mmoja aitwae Fenton naye alisema hivi katika kitabu chake, kuhusu Biblia na mvinyo au divai, “Filipo Sidersky, Mkristo Myahudi, alimwambia mke wa Hamilton kwamba wakati wa chakula cha pasaka Wayahudi walikamua maji ya mzabibu kutoka katika matunda yake na kuweka katika chombo kikubwa.” Tafsiri ya Ferrar Fenton ya 1 Wkor.5:6-8 inasema, “ *hamjui ya kwamba chachu kidogo hulichachua donge zima. Basi jisafisheni mkatoe ile chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo hamkutiwa chachu. Kwa maana pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa sadaka, yaani Kristo. Basi na tuifanye karamu, si kwa chachu ya kale, wala kwa chachu ya uovu na ubaya, bali kwa yasiyochachika ndiyo weupe wa moyo na kweli.*” **Chachuka na kutiwa amira** zina fanana, pia **isiyochachwa** na **isiyotiwa amira**

maneno yote ni sawa, na yanatumika kwakubadilishwa tu. W.F. Jones akiandika zaidi katika karatasi yake anasema, “ *kwa maana Kristo pasaka wetu ametolewa dhavi kwaajili yetu*” (1Wakor. 5:7). Kwaiyo, katika mustari wa 8, waubiri wa injili wanaunga mkono kuendelea kutunza meza ya ushirika bila kuchachuliwa.” Na hiyo ina maanisha isiyo tiwa kituchochote kama nilivyoonyesha. Sasa basi anapaswa kujiuzulu kutika katika ubishi wake juu ya mvinyo mkali (pombe) au abadilishe ubishi wake.

Sasa nahitaji umakini wako kuhusu “swali juu ya kikombe” na J.L. Musgrave. Katika kipeperushi alitoa mdahalo na katika ukrasa wa 1 inatoa mwanga mkubwa, “ chombo kimoja ndugu wamekosea katika kila kitu,Biblia, historia, na wataalam wa dunia.” Kwa mtazamo wa Kibiblia, kihistoria na ushahidi wa kitaalam ambayo nimewakilisha kwenu, na ambayo nitazidi kuwakilisha kwa minajili ya kikombe kimoja, nitawaruhusu wasomi wahukumu ikiwa tumekosea katika kila kitu.

Ukrasa wa 13 anajifanya kumnukuu Yesu, “ hiki (kikombe) ni damu yangu,” lakini Kristo hakusema hivyo. Yesu alisema, “*kikombe hiki ni Agano Jipya*”, na wote tunafahamu kuwa Agano Jipya sio damu yake, pia kikombe sio damu yake, bali ni Agano Jipya (iliyotiwa mhuri) katika damu ya Kristo. Tafsiri ya Moffatt inatoa ufafanuzi katika Luka. 22:20, “*kikombe hiki kinamaanisha agano jipya, iliyo thibitishwa na damu yangu.*” Ukrasa wa 15 Musgrave anasema hivi, “*kikombe hiki (chombo) ni agano jipya.*” Hebu natuangalie kiundani: “*hiki (kikombe) ni damu yangu la agano jipya*” (Math. 26:28). Fikiria kwamba mustari wa kwanza amepatia vizuri (Luka 22:20), lakini katika Math. 26:28 neno “hii” sio “kikombe” mustari wa 29 inasema “**uzao huu wa mzabibu**”. Kwaiyo “*kikombe (chombo) ndiyo agano jipya katika (thibitishwa na) damu yangu*” (Luka 22:20, na “ *uzao huu wa mzabibu ni damu yangu ya ( toleo la mwendo mzuri “inayothibitisha) agano jipya*” (Math.26:28). Hapa Musgrave anasema. “Labda Agano Jipya na damu ya Agano Jipya ni kitukimoja na nisahihi”. Ndiyo, lakini **Agano Jipya inathibitishwa na damu** na pia **damu inathibitishwa na Agano Jipya** hazi fanani. Kristo alisema, kikombe ilikuwa Agano Jipya ( Luka 22:20) na uzao wa mzabibu ilikuwa ni damu (Math. 26:28-29). Kama ilivyo hakikishwa tayari damu ilikuwa kwenye kikombe, lakini haikuwa kikombe chenyeewe.

Sasa hapa tena Musgrave katika ukrasa wa15, katika Kuto. 24:6-8, damu ilikuwa katika mabakuli (wingi); hataivyo, bado ilikuwa ni damu ya agano! Kwa nini damu ya Agano Jipya isiwe katika vyombo nabado iendele kuwa ya agano?” Najibu, kwa sababu Yesu alikuwa nayo kwenye chombo na akasema, **lazima wote mkinywee**” ( Math.26:27; toleo la mwendo mzuri. Lakini vipi kuhusu (wingi) mabakuli mengi yaliyokuwa na damu katika Agano la Kale? Hebu natujifunze kidogo. Toleo la

Mfalme Yakobo inataja mabakuli, lakini neno la Kiyunani iliyotafsiriwa mabakuli hapa ni “aggan”, na katika Wimbo wa Sulemani 7:2, tunasoma “*kitovu chako kina mduara kama bilauri.*” Bilauri inatokana na neno la kiyunani “aggan”. Kama ni umoja hapa, ingekuwa katika Kuto. 24:6. Ukweli wa kutosha upo katika toleo la Myles Coverdale ya 1535, ambayo ninayo, tafsiri ya kwanza ya kiingereza ambayo haijawai kuchapishwa, tunasoma ifuatavyo: “Musa akatwaa nusu ya ile damu, akaitia katika mabakuli, na nusu ya ile damu akainyunyiza juu ya madhabahu” (Kut. 24:6). Unaweza kuona kuwa ni bakuli au bilauri (chombo Fulani au kikombe) ilitumika kama chombo wakati wa Agano la Kale.

Tutasoma sasa katika kitabu cha “tangazo na maandishi yanayo kosoa ya Agano Jipya” na Adam Clark, L.L.D., F.S.A., M.R.I.A., chini ya Math. 26:28-“ Uhakikisho la Agano La Kale lilikuwa lina damu za madume na mbuzi- uhakikisho wa Agano Jipya ilikuwa kwa **kikombe cha uzao wa mzabibu**. Kristo alipoanzisha vielelezo vyote vya Agano Jipya, **anachukuwa kikombe divai**, na anawapa kunywa, na kusema, “*hii ni agano jipya katika damu yangu.*” Katika dibaji hii ya injili anasema, wakati wa kusheherekea chakula chake cha mwisho, Kristo anaita kikombe, “*kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu*” **ishara inayoleta uwakilisho wa agano jipya, iliyo thibitishwa na damu yake**, angalia, Luka 22:20., kikombe ilikuwa ni ishara ya Agano Jipya, na Agano Jipya haikuwa damu, bali ili thibitishwa na damu. Tangazo la Adam Clark ya Luka 22:20. “Haionekani kuwa Bwana aliwapa mkate au kikombe kila mmoja (hakuwagawia kila mmoja): Alimpa mtu aliyekuwa karibu naye, na wakapokezana mmoja baada ya mwingine, walikishiriki wao kwa wao, mustari wa 17. Kwa heshima hii, mtindo uliopo wa kuhudumia Meza ya Bwana haiko sawa sawa na ile iliyoanzishwa kiasili”. Kupitisha vikombe haikuwa njia au mtindo wa asili. Chini ya Luka 22:17 anasema, “Gawaneni hiki kati yenu. Pitisha kikombe kutoka kwa mtu mmoja hadi kwa mwingine.” Hii inatoa uamzi wa kutupilia mbali ubishi wa Musgrave katika ukrasa wa 19 ya kipeperushi chake. Katika ukrasa wa 20-23 amejichanganya mwenyewe katika matumizi ya lugha. Kwanza, anatoa ufafanuzi mzuri juu lugha isio ya kawaida, baadaye anawakilisha ubishi wa chombo kimoja kimakosa. Hatusemi kwamba kikombe cha Bwana hakijulikani. Bali tunasema kikombe cha Bwana ni cha uzao wa mzabibu. Neno kikombe mara nyingine inatumika kama umoja, kama katika 1 Wakor. 11:27, “*Kunywa hiki kikombe cha Bwana*”. Paulo hapa alitaja chombo kupendekeza. Kumbuka, hakutaja kilichomo bali alitaja kitukingine ambayo ilikuwa tayari imeshapendekezwa. Hii ni kulingana tafsiri ya Musgrave juu ya neno metonim katika ukrasa wa 20, Metonim ni lugha ya mfano ambayo kitufulani au wazo inaletwa katika akili, sio kwa kuita yenyewe, bali

kwakuita kitu kingine ambayo inaipendekeza. Sasa neno “kikombe” katika 1 Wakor. 11:27 imetumika kama metonim, chombo iliyoitwa kwa kile ilichonacho ndani yake, lakini kutumika kwake kama metonim haifanyi kuwa metonim kila sehemu, kwasababu Matt. 26:27 neno kikombe inamaanisha kifaa cha kunywea (chombo), Thayer – ukrasa wa 510, 533 na 189. Kikombe hapa ni halisi.

Katika 1Wakor.10:16 chombo na kilichomo vyote kwa ujumla vinamaanisha yale yaliyoonyeshwa hapo awali. Alafu Musgrave anawarukia wayunani katika ukrasa wa 24. “ kwa muyunani! Kwa muyunani!”, pigeni kelele rafiki zangu. Kikombe kimechukuliwa kutoka kwa mfyanzi, ambayo inamaanisha chombo cha kunywea, kifaa ambacho mtu anatumia kwakunywea. Marachache, kama si haba, wanamwambia yeyote “*kikombe*” katika Math.26:39 inatokana na neno la Kiyunani poterion. *Ikiwezekana kikombe hiki* (kikombe, chombo cha kunywea, chombo ambacho mtu anatumia kwa kunywea) *kiniepuke*”. Sikiliza madai ya Clark juu ya hili swala, “ inaonekana kuwa ni uovu kwa mtindo uliopo wa kuadhibu watuhumiwa. **Kikombe iliyo na sumu iliwekwa mikononi mwao na walitakiwa kuinywa.** “...niepuke...”labda hapakuna uwezekano kwa wafungwa wengi walio simama kwenye mustari, ambao wanapaswa kukinywea kikombe hicho, lakini mhukumu anasogeza mbele upendeleo kwa yeyote, kikombe kilipita kwake hadi kwa aliyefuata.” Kwaiyo, inaonekana kuna kikombe halisi inayohusishwa hapa na pia katika ulinganisho wa maneno.

J. L. Musgrave, katika kipeperushi chake “ swali la kikombe” ukrasa wa 33 anajaribu kumpata mtu amsaidie. Anafikiri ni uthibitisho wa ajabu; na nikwaajili yangu,na siyo kwaajili yake. Kumbuka barua kutoka Lexicographer: “ katika toleo la Mfalme Yakobo, neno kikombe imetumiwa ili kumaanisha kitu kilichomo, nikama jinsi mtu anasema, “Alikunywa kidogo mara moja,’ au mwingine anaweza kusema, alipitisha kikombe kwa kila mmoja, na kila mtu akakinywea na kusema, ni jinsi gani hii ilivyo nzuri’ , kwa mtamshi “**hichi**” “**hiki**” inaeleza kitu ambacho kipo ndani ya chombo, na siyo chombo chenyewe.” Lexicographer.

Sasa hiyo ilimuuma na ikanisaidia mimi. Wote walinywea kikombe halisi. Kulikuwa kunakitu chenye incha ndefu inahusishwa hapa, na wote walio kunywa kilicho kuwemo walikinywea. Sawa, hicho ndicho ninachosema kuhusiana na kikombe cha Bwana. Pitisha kikombe kwa kila mmoja na wote wanywe kidogo kidogo. Kila mtu anayekinywea anakunywa kikombe. “*Hiki*” katika Math.26:28, inaeleza kile kilichomo ndani ya kikombe na siyo kikombe chenyewe. Sikuhitaji msada huu, lakini inashukuriwa hataivyo. Ningependa Musgrave angeanza kupitisha kikombe (siyo vikombe) kwa kila mtu na wanywe kidogo kidogo. Katika Marko 14:23, “ *Aliwapa: na wote wakakinywea.*”

Lexicographer akasema “hiki” inaelezea kitu ambacho kimo ndani ya kikombe, na siyo kikombe chenyewe. Sasa Musgrave katika ukrsu wa nne ya kipeperushi chake, alikosea aliposema , “hiki (*kikombe*) ni *damu yangu*.” “Hiki” ingeelezea kitu ambacho kimo ndani ya kikombe na siyo kikombe chenyewe. Kama chombo chenye kina kimetumika Musgrave anaweza kuona ni jinsi gani neno “hichi” inazungumzia kilichomo ndani yake, lakini haioni kwa njia hiyo kama kikombe imetumiwa. Labda kama angeweza “*kikombe*” pale ambapo herufi inasema kina angeweza kuelewa. Anaweza kuelewa kuwa “kunywa kikombe” mtu ni lazima anywe kilichoko ndani ya kikombe cha hasili, lakini tunapo sisitiza kuwa kusanyiko lazima wanywe kile ambacho kipo ndani ya kikombe cha asili “kunywa kikombe” anasema, “sawa, utatakiwa umeza chombo.” Je macho yake yana upofu?

Wakati anapotulia kidogo, tutaangalia baadhi ya historia ya Biblia, na uelewa wa ulimwengu, ambao anafikiria wako kinyume nasi. Eadies Biblical Cyclopedia iliyoandikwa na John Eadies, D.D., L.L.D., chini ya 1 Wakor. 10:16, “ Mkuu wa sherehe alichukua kikombe cha uzao wa mzabibu mkononi mwake na taaratibu akaomba Mungu kwaajili ya kikombe na kwa uruma zake ambazo badaye zili dhihirika. Sasa ilipitishwa kwa wageni wote, ambamo wote walikinywea kwa zamu.” “kili” chukuliwa mkononi mwakwe, “kili” pitishwa kwa wote, na kila mmoja “akaki” nywea kwa zamu.

Sasa kwa kiwango kizuri tutarudi kwa maneno halisi ambayo Kristo alitumia, **poterion**, hili neno limetafsiriwa “*kikombe*” katika kiingereza. Tutaenda kuangalia kitabu cha Agano Jipya cha kiyunani na kiingereza iliyoandikwa na Edward Robinson, D.D., L.L.D, na uangalie kama anakubaliana na Thayer. “poterion, 1. Chombo cha kunywea, kikombe; Math.10:42; 23:25; 26:27; Marko 14:23; Luka22:17, 20; 1Wakor. 11:25. 2. Meton, kikombe kwaajili ya kilichoko ndani ya kikombe, kikombe kimejaa, labda kikombe cha uzao wa mzabibu; cha uzao wa mzabibu ilinyweka pale; Luka 22:20; 1Wakor. 11:25; 10:16.” Kwaiyo ipo katika ushirika “*kikombe*” na “*kilichopo ndani ya kikombe*”, “*kikombe cha uzao wa mzabibu*” (mfano na halisi vyote vimetolewa). Unaweza ukawa na halisi bila kuwa na mfano, lakini pia huwezi kuwa na mfano bila halisi.

Ndugu zangu kwa nini vikombe vinawekwa katika zaidi ya chombo kimoja? Wanasema ni kwaajili ya umati mkubwa wa watu na hatari ya kutokuambukizana magonjwa. Wanatoka nje ya mifano ya Agano Jipya kwa sababu hizi. Unafahamu ya kuwa katika karne ya kumi na tano Wakatholiki kwa sababu hizi walibadilisha ushirika na wakashikilia kikombe kutoka katika utanda? Mbele yangu nina vitabu viwili vya kwao, “Imani ya Mamilioni” na “Imani ya Mababu zetu” ukianzia ukrasa wa 223 ya kitabu cha kwanza na ukrasa wa 306 ya barua tunasoma ifutavyo: “ kwa nini mnawapa ushirika kwa wakuu”, aliuliza mtu



aliyekuwa na haja hivikaribuni, “ katika kiwango cha mkate na sio katika kiwango cha uzao wa mzabibu vilevile? Hatari ya kuharibu damu ya thamani; ugumu wa kupokea sakramenti, chini ya mwongozo uzao; na hatari ya afya kwa kunywea kikombe ambacho kimeonjwa na midomo iliyoathirika. Jinsi swali linavyo husu nidhamu, kanisa inafanyia mazoezi haki yake kama muongozo wa Sakramenti kuiga mtindo wake wa kuzihudumia hadi kiwango cha kubadilika. Itakuwa haina ladha, hataiuyo, kwa washirika wengi kunywa kwa mafanikio katika kifaa hicho hicho. Ambayo hawezi kuepukwa ikiwa Sakramenti ili tumika katika mitindo yote; kwaiyo, katka karne ya kumi na tano aliondoa kikombe. Wakati wa protestanti wanazingatia kikombe kama sehemu muhimu katika ushirika, hawaonekani katika matukio mengi, dhahiri kuwa kutakuwa na nini katika kikombe.” Wakatholiki wanatoa kikombe kwa mtu mmoja badala ya kuwapa wote kama jinsi Yesu alivyo fanya ( Math. 26:27; Marko 14:23) kwa sababu wakifanya kama Yesu alivyofanya itakuwa **hatari na kukosa ladha, hataiuyo, kwa washirika wengi kunywa kwa mafanikio kutoka katika chombo hicho hicho ambayo haiwezi kuepukika.** Wakatholiki walifahamu kuwa Yesu alitumia kikombe kimoja, lakini kwa sababu hizi walibadilisha mtindo wa kushiriki meza ya Bwana. Kwa kiwango Fulani ni wawazi kwa kukiri kwamba walibadilisha mfumo. Ndugu zangu vikombe vinakubaliana na wakatholiki katika hatari na kukosa ladha kwa kutumia kikombe kimoja, lakini wanachukua hatua tofauti ya kubadilisha ushirika. Wanaanzisha vikombe vingi ili kuwa na kimoja kilichozoeleka. Katika mtindo huu hawana Biblia kama wakatholiki nao wanavyofanya katika ushirika wao, lakini ni afadhali nifuate nyayo za Yesu ( Yoh. 14:6). Sidhani kwamba ni hatari kufanya kama Alivyo sema. Lakini kwa wale wanao waamini wanadamu kuliko Mungu, ninatoa yafuatayo:

## USHIRIKA WA USAFI

(Imenukuliwa kutoka katika jarida la Pathfinder, Washington D. C., Machi 20, 1944).

Mila safi ya ushirika wa kikombe ambayo inaturudisha nyuma katika “ chumba cha juu” kule Yerusalem imeachwa huru marazote kwa “kubeba vijidudu” kwa uchunguzi wa kisayansi wa maprofesa wawili wa Chicago.

Katika yaarifa ya uandishi wa kuathirika kwa ugonjwa, Dk. William Burrows, na profesa mhusika wa mambo ya vijidudu, na Dk. Elizabeth Hammons, mwalimu wa Walter G. Zoller kiliniki ya meno, anaonyesha kuwa chuma kizito, hasa, fedha ilitambulika zamani kuwa ina athari ya vijidudu, kwaiyo kikombe cha kawaida haisambazi magonjwa. “

magonjwa yanayo fahamika kati ya migahawa inayo fahamika, na kikombe cha ushirika cha dhahabu,” wanasayansi walieleza, vijidudu viliua mwenendo wa dhahabu, na umakini ambao Sakramenti inavyo udumiwa.”

(Kama vikombe ndugu zangu inaweza kutoa udhibitisho mwingi kwamba vikombe vilikuwa salama, kama jinsi tu nilivyo na kikombe kimoja, tungeharibika zamani sana, kama kikombe kimoja kina virusi.) Kama kuna mtu wa vikombe vingi ambaye anaweza kutoa uthibitisho mwingi wa Kibiblia, na kihistoria kwamba Kristo alitumia vikombe, jinsi nilivyo thibitisha kwa kimoja, sio tu nitamshangaa, bali pia nitampa zawadi ya dola mia moja.

Hebu tuangalie baadhi nukuu ya ushirika katika tafsiri zingine tofauti na Tafsiri ya Mfalme Yakobo. Lakini wengine watasema kuwa hawaamini katika tafsiri zingine. Kwa nini? “oh!” wanasema, “ ilikuwa ya kwanza na lazima Mungu alitaka tuwenayo.” Sawa, hawako sahihi, kwa sababu nina tafsiri nne za Kiingereza ya zamani kuliko tafsiri ya Mfalme Yakobo na labda kuna zingine pia. Hebu tusome hizi.

(Toleo la Wycliffe, 1389 A.D)- Math.26:27, “na ali chukuwe kikombwe, bawade ye kushokoro, akawapa, akiseme, nywene nyota na wote wakakinywea.” Luka 22:20, na baada ya hapo akakitwa kikombe, akaseme kikombwe hikw ni aganojipe katika damu yangu iliyo mwageki kwaajili yenu.

(Toleo la Tyndale, 1526 A.D)- Math.26:27, “na akachokoa kukombe, akashukuru, akawapa, akaseme, nyweni katika hiki kila moja.

(Toleo la Coverdale, 1535 A.D) Math. 26:27 “na akachukia kikombe, akashukuru, akawapa, aseyema; nywene nyoti.” Marko 14:23, “ Na akachokoa kikombe, akashokoro, akawape, na wote wakakinywea.

Nimeacha maneno kama jinsi ilivyo katika Biblia hizi za zamani. Kiingereza ya zamani ilikuwa haina maneno yaliyo nyooka. Mtu kama hawezi kusoma, nitatamka maneno haya kwa njia ya kisasa kwaajili yao. Toleo la Chailover Rheims, 1582 A.D Marko14:23, “ na akachua kikombe, akashukuru, akawapa, na wote wakakinywea.”

(Toleo la Mwendu mzuri)- “Na **akachukua kikombe cha uzao wa mzabibu** akiisha kushuru akawapa **na wote wakakinywea.**” 1 Wakor.11:25, “Kikombe hiki ni makubaliano mapya kwaajili ya damu yangu.”

(Tafsiri ya Moffatt) 1 Wakor.11:25, “ **kikombe hiki kinamaanisha agano jipya katika damu yangu.**

(Tafsiri ya karne ya ishiringi) Marko 14:23, “ **baadae akakichukua kikombe na wote wakakinywea.**”Luka 22:20, “**kikombe hiki ni agano jipya iliyotengenezwa na damu yangu.**” ( Toleo la American



Standard ) Marko 14:23 **Alichukua kikombe na wote wakakinywea.”** ( toleo la kawaida ya 1946)- Marko 14:23- “ **Alichukua kikombe na wote wakakinywea.”**

Kwa uthibitisho huu wote kwamba Kristo alichukua kikombe na wote wakakinywea, tunaweza kusemaje tunamfuata Kristo ilihali tuna chukua vikombe vingi na kuvinywea? (Math. 26:27; Marko 14:23; Math.28:20; 2Yoh.6:9; 2Tim. 3:13-17).





